**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# MKATABA WA UFADHILI WA MTUMISHI KUHUDHURIA MASOMO YA KUJIENDELEZA KITAALUMA

## NOTISI

1. Mkataba huu utatumika endapo Mfadhiliwa atahudhuria masomo kwa kozi ya muda wa zaidi ya miezi tisa kwa kufadhiliwa gharama zote au sehemu ya gharama za mafunzo na Serikali.

2. Mfadhiliwa anayeenda kusoma kozi (za aina yoyote) za muda mrefu za elimu ya juu ndani na nje ya nchi, inazozidi muda wa miezi tisa, atatakiwa kuwa na angalau wadhamini wawili wa kutia saini mkataba huu.

3. Kila mdhamini atatakiwa kuwa na barua ya kukubali kumdhamini Mdhaminiwa/Mfadhiliwa na itakuwa sehemu ya mkataba kati ya Serikali na Mfadhiliwa.

**MKATABA WA UFADHILI WA MASOMO**

Mkataba huu umefanyika leo tarehe …………………. Mwezi ………………20…….

Kati ya

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Afya, Mji wa Serikali – Mtumba, Barabara ya Afya, S.L.P 743, 40478 Dodoma (ambaye katika mkataba huu atatambulika kama “Serikali”) kwa upande mmoja;

Na

……………………………………………… Mwajiriwa wa ………………………………… ambaye kituo chake cha kazi ni ………………………………………. wa S.L.P ……………., ………………………….. (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**Mfadhiliwa**”) kwa upande mwingine.

**KWA KUWA:** Serikali imeamua kuwaendeleza watumishi kitaaluma kwa kutoa ufadhili kwa watumishi wenye sifa zinazotakiwa;

**NA KWA KUWA;** Mfadhiliwa ana sifa zinazotakiwa katika kupata ufadhili huo kutoka Serikalini;

**HIVYO SERIKALI NA MFADHILIWA kwa pamoja** wanakubaliana kama ifuatavyo;

1. Tafsiri
   Kwa madhumuni ya mkataba huu,
   **(a) Mdhamini** maana yake ni mtu yeyote mwenye sifa ya kumdhamini mtu isipokuwa mwajiri; na

   **(b) Serikali** maana yake hujumuisha mwajiri.

**2.** Kwamba, Mfadhiliwa anakubali kufadhiliwa na Serikali kwa kusoma kozi ya ………………………………………………………. katika chuo cha …………………………………..

3. Na kwamba, Mfadhiliwa anakubali kuwa hatabadili kozi au kuhama chuo alichowasilisha awali kwa ajili ya ufadhili bila mabadiliko au uhamisho huo kuidhinishwa na Serikali kupitia mamlaka inayomfadhili.

4. Na kwamba, Mfadhiliwa anakubali kuwa ufadhili wake utaanza rasmi kuanzia siku jina lake litakapotangazwa rasmi kupata ufadhili na ufadhili huo hautajumuisha madeni ya nyuma yanayotokana na masomo kabla mfadhiliwa hajapata ufadhili.

5. Na kwamba, Mfadhiliwa anakubali kuwa ufadhili atakaopata hautakuwa na ufadhili wa muda wa ziada na iwapo atashindwa kuhitimu mafunzo yake ndani ya muda uliopangwa wa kuhitimu katika taaluma anayosomea atajigharamia mwenyewe kwa muda wote ambao chuo husika kitamuongezea ili aweze kuhitimu.

6. Na kwamba, Mfadhiliwa anakubali kuwa ikitokea amebadili kozi au amehama chuo alichowasilisha awali kwa ajili ya kupewa ufadhili na kusoma kozi nyingine au kwenda chuo chenye ada zaidi ya kile kilichokubaliwa awali na Serikali, Serikali itasitisha ufadhili huo na atalazimika kurejesha gharama zilizolipwa katika chuo anachohama.

7. Na kwamba, Mfadhiliwa atatakiwa kuitaarifu Serikali katika suala lolote linalohusiana na masomo yake ikijumuisha kuahirisha, kusitisha masomo kwa sababu yoyote iliyothibitishwa, kuongezwa kwa muda wa masomo au kushindwa kuendelea na masomo kwa sababu ya kutofaulu masomo kwa mujibu wa kanuni na taratibu za chuo husika.

8. Na kwamba, Mfadhiliwa anakubali kuwa amepata ufadhili mwingine tofauti na ule wa Serikali, kabla ya kuanza masomo au akiwa masomoni, ataitaarifu Serikali mara moja ili ufadhili wa Serikali usitishwe; na iwapo ikibainika kuwa ana ufadhili mwingine na ule wa Serikali, Serikali itasitisha ufadhili wake na atatakiwa kurejesha fedha ambayo tayari amelipiwa kama ufadhili iwapo kama ufadhili huo unahusisha gharama ambazo Serikali imekuwa ikigharamia.

9. Na kwamba, Mfadhiliwa anakubali kurudi katika kituo chake cha kazi cha ……………………………………………………….. ambacho ametoka kwenda masomoni na kuendelea kubaki hapo kwa kipindi cha miaka mitano bila kuomba kuhama isipokuwa tu Serikali ikiamua kumbadilisha kituo cha kazi kwa kadiri itakavyoona inafaa kwa manufaa ya umma.

10. Mfadhiliwa aliyepata ufadhili kwa ajili ya masomo ya ubingwa na baadae kuunganisha kwa ufadhili wa Ubingwa Bobezi (Super Speciality) atalazimika kurudi kituo chake cha kazi baada ya kuhitimu na kubaki kituo hicho kwa kipindi cha miaka saba bila kuomba kuhama au hadi Serikali itakavyoamua vinginevyo.

11. Na kwamba, Mfadhiliwa atatakiwa kuwasilisha taarifa ya maendeleo kutoka kwenye chuo anachosoma kuhusu kuendelea na masomo kwa mwaka mwingine wa masomo.

12. Mfadhiliwa anakubali kuwa ikitokea masharti ya mkataba huu yamekiukwa, tofauti na masharti ya kuendelea kubaki kituo chake cha kazi baada ya kuhitimu masomo yake, Mfadhiliwa yeye pekee au na Mdhamini wake kwa pamoja

watawajibika kurejesha gharama zote zilizolipiwa na Serikali kwa ajili ya masomoni yake.

13. Na kwamba, mkataba huu utatekelezwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania zinazohusu mikataba na Utumishi wa Umma.

Mwajiri anathibitisha kuwa Mfadhiliwa ana Ufadhili/hana ufadhili wowote kutoka kwa Mwajiri au mfadhili yeyote (kata isiyohusika).

Jina la Mwajiri:…………………………. Saini:……………………..…………
Tarehe…………………………….….... Muhuri: ………………………………..

Kwa kukubaliana na masharti ya mkataba huu, Mfadhiliwa na wadhamini wake wote kwa pamoja wameweka sahihi zao kama ifuatavyo;

**Mfadhiliwa:**
**Jina:**
**Anwani:**
**Sahihi:**
**Barua pepe:**
**Namba ya simu:**

**MDHAMINI WA KWANZA**
Jina: ……………………………………..
Anwani:…………………………………..
Sahihi: …………………………………...
Namba ya simu: ……………………….
**Muhuri wa Hakimu/Wakili/Kamishna wa Viapo**

**MDHAMINI WA PILI**
Jina: ……………………………………..
Anwani: …………………………………
Sahihi: …………..……………………
Namba ya simu: ……………………….
**Muhuri wa Hakimu/Wakili/Kamishna wa Viapo**

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU**
**Kwa niaba ya Serikali:**
**Jina:**
**Sahihi:**
**Cheo na Muhuri wa Ofisa:**
**Tarehe:**

Anwani ya Mdhamini
Jina la Mdhamini,
S.L.P ………………..
…………………(Mji)

Kumb. Na. …………………………… Tarehe……………..

Anwani ya Serikali (Mfadhili)
………………………………...
S.L.P …………………………
MJI……………………………

**YAH: KUKUBALI KUMDHAMINI ………………………………….. ANAYEPEWA UDHAMINI NA SERIKALI**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Mimi, ……………………………………………… (Jina) nakubali kwa hiari yangu kumdhamini ………………………………………………… (jina la Mdhaminiwa) ambaye amepata ufadhili wa Serikali kwenda masomoni kusoma kozi ya ……………………………… katika chuo cha …………………………………………………

3. Kwa barua hii, niko tayari kuwajibika endapo Mfadhiliwa atakiuka masharti ya Mkataba wa Ufadhili ikiwa ni pamoja na kurejesha fedha zote atakazokuwa amelipiwa Mfadhiliwa kwa ajili ya masomo yake endapo itatakiwa kuwa hivyo.

4. Nashukuru kwa ushirikiano wako.

Jina:…………………………………
Sahihi: ………………………………….
Namba ya simu:………………………………..